26. Makadirio ya mapato na matumizi.
27. Hesabu na u, kaguzi wa hesabu.
28. Taarifa, ya mwaka.
29. Uwezo wa kutoza ushuru.

SEHEMU YA SITA

MASHARTI YA KAWAIDA

30. Dhaynana ya wajumbe, n k.
31. Uwezo wa kupekua.
32. Adhabu ya junila.
33. Kuhozi.
34. Kosa kutendwa na shirika.
35. Muajiri au msimamizi kuhusika na kosa.
36. Utangazaji wa kanuni au maagizo.
37. Jukumu la kuthibitisha.
38. Msamaha.
39. Waziri kuweka k .

SEHEMU YA SABA

KUVUNJWA KWA BARAZA LA YAMUWA NA MATOKEO YAKE

40. Ufafanuzi.
41. Kuhawifisha rasilmali na dhima za Baraza la Kahawa.
42. Matokeo ya kuvunjwa kwa Baraza la Kahawa.

SEHEMU YA NANE

KUFUTWA KWA SHERIA YA KAHAWA YA ZAMANI NA MATOKEO YAKE

43. Kufutwa kwa Sheria ya Kahawa ya ziani, Sura ya 438.
44. Masharti ya Sheria ya Kahawa ya zamam yatakayoendelea kutumika.
45. Masharti ya muda.

NYONGEZA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA. 5 YA 1977

NAKUBALI

J. J. K. Nyerere
Rais

22 Juni, 1977

Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kahawa ya Tanzania na kueleza kazi na madaraka ya Mamlaka; kuweka masharti kuhusu uthibiti, urekebishaji na, ustawishaji bora wa uchumi wa kahawa; kuifuta He Sheria, ya Kahawa ya zamani na kueleza mambo mengineyo yanayohusika na uchumi wa kahawa

[.....]

SHERIA HII ImETuNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEW YA KWANZA

UTANGULIZI

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Kilimo na Uchumi wa Kahawa, jinana mwaka 1977 na itaanza, kutunika rnamo tarehe itakayowekwa namwanzowa kutuffi'a
 - 2.-(1) Katika Sheria hii, ila iwapo maelezo yake yatahitaji tafsiri Ufafanuzi nyingineyo-
 - „maniakal, maana yake ni Mamlaka ya Kahawa ya Tanzania yaliyoanzishwa na fungu la 3;
 - "Baraza" maana yake ni Baraza la Wakurugenzi wa Mamlaka Miloanzishwa chini ya fungu t'a 5;
 - "kahawa" maana yake ni kahawa yenye maganda na buni safi;
 - "Mkurugenzi" maana yake ni ofisa mshika madaraka ya idara katika Wizara ya Kilixno inayosimamia mastawisho ya mazao;
 - "tarehe ya kuanza" maana yake na tarehe ya kuanza kutunlika kwa Sheria hii;
 - "mkulima" maana yake m, mitu yeyote anayelima kahawa;
 - "Waziri" maana yake ni Waziri wa Kilfino;
 - „utengenezaji" maam yake ni kutengenem kahawa kwa namna yoyote
- (2) "Ununuzi" na „uuzaji" ni pamoja na kutaka kuuza au kununua na vile vile shughuN yoyote ambayo kitu kinachoshughulikiwa kita-kwenda kwa mnunuzi.

SEHEMU YA PILI

MAMLAKA YA KAHAWA YA TANZANIA

Kuanzishwa
kwa
Mamlaka ya
Kahawa ya
Tanzania

3.- (1) Kutakuwa, na Mamlaka, ambayo yataitwa Mamlaka ya Kahawa ya Tanzania.

(2) Mamlaka haya yatakuwa ni shirika, la kisheria na-

- (a) yAtakuwa yakudumu na yatakuwa na muhuti wake rasmi;
- (b) kwa jina, lake hilo yatawca kushtaki, na pia, kushtakiwa;
- (c) kwa kufuata Sheria, hii, yataweza, kushika, kununua au kupata au kusarifu mali..yoyote inayoharnishika, na isiyohamishika kwa ajili ya kuendesha kazi ambazo yarnepewa, chini ya Sheria hii au sheria, nyingineyo yoyote ya maandishi.

Kazi za
Mamlaka

4.- (1) Kazi za Mamlaka zitakuwa hizi-

- (a) kustaw.isha kahawa, kuinua hali na kuulinda uchumi wa. kahawa;
- (b) kutayarisha, kutekeleza, kudhibiti na kusimamia mipango inayo. husika na ustawi wa uchumi wa, kahawa;
- (c) kuendesha, amapeke yake au kwa kushirikiana na mtu mwingine yeyote, kazi ya kulima na kutoa zao la kahawa, kazi ya kuitengeneza kahawa, na kazi au shughuli nyingine zozote zinazoclekeana au zinazohusiana na kazi hizo;
- (d) kusimamia, uuzaji na upelekaji nje wa kahawa;
- (e) kurnshauri Waziri juu ya hatua zifaazo kwa ajili ya kuinua na kulinda uchumi wa kahawa;
- (f) kushiriki katika, kuinua au kudhibiti utoaji au uuzaji wa, kahawa kwenye shirika lolote la kimataifa au kuingia, katika mapatano yanayohusika na mambo hayo.

(2) Bila ya kuathiri kazi za jumla zilizoelezwa katika, kifungu cha, (1), na kwa kufuata waagizo yoyote ya Waziri, maagizo ya jumla au maagizo maalum, Mamlaka haya yaweza hasa-

- (a) kuthibiti na, mara kwa mara, kuweka bei zitakazolipwa kwa ajili ya kahawa au mazao yatokanayo na kahawa yanayosafirishwa au kuuzwa kwa ajili ya viwanda vya hapa nchini na yanaweza kuzingatia bei hizo kwa namna yatakavyoona inafaa;
- (b) kurekebisha uuztiji wa kahawa na mazao yatokanayo na kahawa kwa matunfizi ya Jamhuri ya Muungano.
- (c) kutoa huduma kwa ajili ya kustawisha uchumi wa kahawa pamoja na-
 - (i) kuanzisha mashamba ya kahawa ya niaonyesho kwenye sehemu zinazolihiwa kahawa;
 - (ii) kusimamia ukulima mimea ya kahawa na uvunaji au utengenezaji wa. kahawa unaofanywa na wakulima wa kahawa;
 - (iii) kukagua, kupambanua na kuweka daraja za kahawa,.

- (iv) kufanya mipango kwa ajili ya uuzaji, uwekaji na uchukuzi wa kahawa;
 - (v) kutoa huduma, nyinginezo za kitaalam kama zitakazohitajiwa na wakuhma, kwa ajili ya kulima mazao yasiyokuwa kahawa;
 - (d) kufanya uchunguzi au kulipia uchunguzi katika utoaji, uuzaji na utumaji wa kahawa na mazao, yatokanayo na kahawa;
 - (e) kupata na kushika masilahi, kwa mapatano katika kampuni yoyote au shirika linaloshughulika na kahawa au mazao yatokanayo na kahawa;
 - (f) kusimamia na kuendeleza shughuli za shirika lolote la umma au kampuni yoyote ambayo masilahi yake yamewekwa au yamepatikana na Mamlaka chini ya Sheria hii. iwe shughuli hiyo inahusika na kahawa au mazao yatokanayo na kahawa au vinginevyo;
 - (g) kufungua matawi yake katika Jamhuri ya Muungano au mahali penginepo;
 - (h) kwa kufuata Sheria hii na kwa kufuata kanuni zozote zilizo fanywa na Waziri kuhusu utoaji wa leseni chini ya fungu la 39, yatatoa leseni kuwapa watu kwa ajili ya kutengeneza kahawa. kutoa mazao yoyote yatokanayo na kahawa au kufanya shughuli yoyote nyingineyo inayohusika na kahawa;
 - (i) kutenda vitendo vyote na mambo yote ambayo Baraza linaona kuwa ni ya lazima ili kudumisha na kukuza sifa bora ya Mamlaka, na kupata imani ya umma na kuinga au kupunguza hasara kwa Mamlaka;
 - (j) kutenda jambo lolote au kujitia katika shughuli yoyote ambayo, kwa maoni ya Baraza, inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Mamlaka chini ya Sheria hii.
- (3) Kwa makusudi ya kutekeleza kazi zake, Mamlaka yatahesabiwa kuwa yanayo kila aina ya leseni, ruhusa na kila idhini ambayo yaweza kuhitajiwa na Sheria hii kwa ajili ya jambo, lolote linalohusika na uchumi wa kahawa.

5.-(1) Litakuwapo Baraza la Wakurugenzi wa Mamlaka ambalo kwa kufuata Sheria hii, litatekeleza kazi na kusimamia shughuli na mambo mengineyo ya Mamlaka.

(2) Yale masharti yaliyoko kwenye Nyongeza ya Sheria hii yatahusu kwenye katiba na maendeleo ya Baraza na pia kwenye Baraza lenyewe.

(3) Waziri, kwa amri atakayoitangaza katika Gazeti la *Serikali*, aweza kusahihisha, kugeuza au kubadilisha masharti yote au sharti lolote kwenye Nyongeza ya Sheria hii.

6. Waziri awoze kulipa Baraza maagizo kwa jumla au maagizo maalum kuhusu kazi zozote zinazotendwa na Mamlaka chini ya Sheria hii, na Baraza litatilia nguvu kila agizo lililopewa

Waziri
aweza kutoa
maagizo kwa
Mamlaka
Kanuni na
maagizo ya
Mamlaka

7.-(1) Itolewapo kanuni yoyote au maagizo yoyote na Mamlaka chini ya Sheria hii, basi Baraza litafikisha yaliyomo kwenye kanuni hiyo au maagizo hayo kwa wanaohusika kwa namna litakavyoamua Baraza mara kwa mara:

Isipokuwa kwamba itafahamika kuwa watu wote wameyajua yaliyomo kwenye kila amri au kwenye maagizo yote iwapo yatatanzwa katika *Gazeti la Serikali*.

(2) Mtu yeyote atakayekosa kufuata amri yoyote au maagizo yoyote yaliyotolewa na Mamlaka atakuwa ametenda kosa.

SEHEMU YA TATU

ULIMAJI NA UTENGENEZAJI WA KAHAWA NA SHUGHULI NYINGINEZO ZA KAHAWA

Maeneo ya kulimwa Kahawa

8.-(1) Waziri baada ya kushauriana na Baraza, na kwa kutangaza kanuni katika *Gazeti la Serikali*, aweza kulitamka eneo lolote au maeneo yoyote katika Jamhuri ya Muungano, kuwa ni eneo au maeneo inapolimwa kahawa au ambapo kahawa italimwa. Eneo litakalotamkwa hivyo litajulikana kuwa ni "eneo la kulimwa kahawa".

(2) Waziri, kila atakapotoa amri chini ya kifungu cha (1), basi Baraza litachukua hatua zote za lazima ili kuitilia nguvu kanuni hiyo.

Mamlaka yaweza kutoa maagizo

9.-(1) Mamlaka, kwa idhini ya Waziri, yaweza kutoa maagizo-

- (a) kuhusu wakati na jinsi ya kutayarisha ardhi kwa ajili ya kupanda kahawa na kuhusu wakati na jinsi ya kuvuna, kukausha, kuweka, kutengeneza na kuuza kahawa;
- (b) kuhusu aina moja au zaidi za kahawa zitakazopandwa katika eneo moja au zaidi ambayo Mamlaka yatataja katika maagizo hayo;
- (c) kurekebisha daraja za kahawa, kufunga katika magunia na kuuza kahawa;
- (d) kurekebisha utengenezaji, uwekaji na uuzaji wa mazao yanayotokana na maganda ya kahawa.

(2) Maagizo yaliyotolewa chini ya fungu hili yatataja aina ya wakulima au watengenezaji wa kahawa ambao itawabidi wayafuate maagizo hayo, na iwapo maagizo yoyote hayataji aina ya wakulima au ya watengenezaji kahawa ambao itawabidi wayafuate, basi itabidi maagizo hayo yafuatwe na wakulima wote wa kahawa na watengenezaji wote wa mazao yatokanayo na kahawa ambao wanahusika.

(3) Mtu yeyote atakayetenda kinyume cha maagizo, au atakayekosa kufuata maagizo yoyote yaliyotolewa na Mamlaka chini ya fungu hili atakuwa ametenda kosa na iwapo ataonekana ana hatia itabidi atozwe faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa gerehani kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au kupewa adhabu zote mbili, faini hiyo na kifungo hicho.

Masharti ya kupanda kahawa

12.-(1) Mamlaka yaweza kuweka masharti kwamba mimea mipya ya kahawa isipandwe na wakulima isipokuwa mimea iliyopatikana kutoka kwa Mamlaka au mimea ya aina itakayotajwa na Mamlaka kutoka mahali popote.

(2) Iwapo Mamlaka inatoa maagizo chini ya fungu hili itafanya mipango yote inayolazimika ili kuhakikisha kwamba inapatikana mimea ifaayo kupowa wakulima wanaohusika.

11.-(1) Mkurugenzi kwa agizo litakalotiwa sahihi yake, na kwa kusudio la kuzuwia au kukomesha, kuingia au kuenea kwa wadudu, wowote waharibifu au maradhi ya mimea ya kahawa au kahawa yenyewe kwenye eneo lolote lililotajwa katika, agizo hilo, aweza-

Kuzuwia
maradhi

- (a) kusema kwamba ndani ya eneo hilo mumea wowote uliotajwa katika, agizo, hilo ungolewe na uzikwe ardhini na mtu yeyote mwenye kuimiliki au mwenye madaraka, nayo, na kwamba ma tunda, yote au matunda yoyote ya kahawa au takataka za kahawa zichomwe moto;
- (b) kumtaka mkulima yeyote wa kahawa katika eneo hilo avune kahawa yake kwa haraka, iwapo Mkurugenzi ataona kuwa iko tayari kuvunwa;
- (c) kupiga marufuku kwamba, kabla ya tarehe iliyotajwa katika, agizo, mtu yeyote asipande mimea yoyote ya kahawa ndani ya eneo hilo au zao lolote lililotajwa katika, agizo hilo ambalo inajulikana kuwa linaweka wadudu harabu au maradhi ya kahawa;
- (d) kupiga marufuku uhamishaji wa kahawa yoyote mbichi au mmea wowote au kitu chochote chenye kahawa mbichi au kitu chochote ambacho, kwa maoni yake, kinaelekea kuweka wadudu waharibifu au maradhi ya kahawa, kutoka, katika, eneo, hilo bila ya ruhusa ya maandishi iliyotiwa sahihi naye.

(2) Mtu yeyote atakayeenda kinyume cha agizo au atakayekosa kufuata agizo lolote lililotolewa chini ya fungu hili atakuwa ametenda kosa.

(3) Iwapo mtu yeyote atakosa kutekeleza masharti ya agizo lolote lililotolewa chini ya fungu hili, basi Mkurugenzi, baada ya kumpa taarifa ya maandishi ya siku zisizopungua saba kuhusu nia yake ya kumchukulia hatua, atamchukulia hatua zinazolazimika, na kwa hali hiyo, mkosaji, bila ya kujali adhabu yoyote anayostahili kupewa kwa sababu ya kosa lake, itambidi alipe gharama zote za hatua zitakazochukuliwa, gharama ambazo atadaiwa na Serikali.

12.-(1) Bila kuathiri masharti ya, kifungu cha (2) na cha (3), Mamlaka inawoza, kwa idhini ya Waziri, kwa amri itakayotangazwa katika Gazeti *la Serikali*, kupiga marufuku kwa mtu yeyote kuuza, kununua, kuweka, kukodisha, kuweka rehani, kusafirisha, kutengeneza, kupeleka nje ya nchi, kuingiza nchini au kwa nia yoyote, kujishughulisha na kahawa au na mazao yatokanayo na kahawa yaliyotaiwa katika agizo, hilo, au kuingiza nchini kitu chochote kinacho tumiwa katika kutengeneza mazao, yoyote ya kahawa yaliyotajwa katika agizo hilo.

Mamlaka
inaweza
kuweka
masharti juu
ya shughuli
za kahawa

- (2) Hakupa jambo. lolote katika kifungu cha (1) litakalohusika na-
 - (i) Mamlaka;
 - (ii) ajenti wa Mamlaka;
 - (iii) mtu aliyeruhusiwa na Mamlaka kwa Maandishi;
 - (iv) mkulima wa kahawa, kuhusu uzaji au uwekaji wa kahawa yake;
 - (v) mtengenezaji mazao ya kahawa kuhusu mazao yoyote yato kayo na kahawa:

Isipokuwa kwamba Mamlaka yaweza kurekebisha na kudhibiti shughuli yoyote katika shughuli zilitajwa kwenye kifungu hicho.

(3) Hakuna agizo lolote, litakalotolewa chini ya fungu hili, ambalo litahusika na-

- (a) uuzaji wowote wa reja reja au uwekaji au usafirishaji wa kahawa kwa ajili ya uuzaji wa reja reja; au
- (b) kiasi chochote cha kahawa au cha zao litokanalo na kahawa kilichonunuliwa na mtu yeyote kwa ajili ya matumizi yake mwenyewe au matumizi ya watu wa nyumbani mwake au watu wanaomtegemea yeye, au na uwekaji au usafirishaji wa kiasi hicho cha kahawa au, kadri itakavyokuwa, zao la kahawa.

SEHEMU YA NNE

UUZAJI NA USAFIRISHAJI WA KAHAWA

Masharti ya kusafirisha kahawa

13.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafirisha kahawa au mazao yatokanayo na kahawa isipokuwa Mamlaka yenyewe au kampuni ndogo ya Mamlaka iliyowakilishwa na Baraza kutenda hivyo.

(2) Mtu yeyote atakayetenda kinyume cha kifungu cha (1) atakuwa ametenda kosa na iwapo atakayekana na hatia itahadi, atozwe faini isiyozidi shilingi laki moja au kufungwa gereza kwa muda usiozidi miaka mitano au kupewa adhabu zote mbili, faini hiyo na kifungu hicho,

Mamlaka ndio mnunuzi pekee wa kahawa

14. Bila kuathiri masharti ya fungu la 15, Mamlaka yatakuwa ndio mnunuzi pekee wa kahawa katika Jamhuri ya Muungano, na kwa ajili hiyo, yataanzisha vituo vya ununuzi ambako wakulima wataweza kuuza kahawa yao kwa Mamlaka.

Maagizo juu ya uuzaji wa lazima

15.(1) Mamiaka, kwa idhini ya Waziri, yaweza kutoa agizo la kuwataka wakulima wa kahawa kwenye eneo lolote litakalotajwa, kuuza kahawa yao au mazao yatokanayo na kahawa kwa mtu fulani au idara fulani itakayotajwa kwa ajili hiyo katika agizo hilo.

(2) Mamlaka, katika agizo lolote lililotolewa chini ya fungu hili yaweza kumsamehe mkulima yeyote au aina yoyote ya wakulima wasihusike na masharti yote au sharti lolote la agizo hilo.

(3) Kila agizo litakalotolewa na Mamlaka chini ya fungu hili litatanzwa katika *Gazeti la Serikali*.

Kima cha chini cha bei ya kahawa

16.-(1) Bila ya kuingilia uwezo, uliotolewa na fungu la 4 (2) (a), Mamlaka, baada ya kushauriana na idara nyinginezo zozote za serikali zinazohusika na bei za mazao ya kilimo, kwa kutoa, agizo katika *Gazeti la Serikali*, inaweza kuweka kima cha chini cha, bei, ambayo, kwayo kahawa yoyote au mazao yatokanayo na kahawa yataweza kununuliwa katika hatua yoyote ya kuuzwa kwake, na ni marufuku kwa mtu yeyote kununua kahawa yoyote au mazao yoyote yatokanayo na kahawa yaliyotajwa katika agizo hilo kwa bei ya chini zaidi ya ile bei iliyokwishawekwa.

(2) Bila ya kujali kifungu cha (1), Waziri akiona kuwa kutenda hivyo ni kwa masilahi ya taifa, kwa agizo la mandishi litakalotiwa sahihi naye ataweza kuweka bei zisizokuwa chini ya kiina cha chini cha bei zilizowekwa na Mamlaka ambazo kwazo kahawa au mazao ya kahawa yataweza kununuliwa kutoka kwa wakulima.

(3) Mtu yeyote atakayenunua kahawa yoyote au mazao yatokanayo na kahawa yaliyotajwa katika agizo hilo kwa bei ya chini zaidi kuliko atakuwa ametenda kosa na iwapo ataonekana ana hatia itabidi atozwea faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa gerezani kwa miezi kumi na mbili au kupewa adhabu zote mbili, faini hiyo na kifungo hicho.

17.-(1) Mamlaka, kwa kutoa taarifa ya maandishi, yaweza kumtaka mtu yeyote apeleke kumbukumbu au habari kuhusu utoaji akiba utengenezaji, uwekaji, usafirishaji, ununuzi au uuzaji wa kahawa au kitu chochote kinachotumiwa katika kutengeneza mazao yoyote yatokanayo na kahawa.

kumbu-
kumbu na
habari

(2) Kila taarifa itakayotolewa chini ya fungu hili itataja jambo linalotakiwa katika kumbukumbu hiyo au katika habari hiyo na pia muda ambao kumbukumbu hiyo au habari hiyo inatakiwa ipeleke na jinsi ya kuipeleka.

(3) Mtu yeyote atakayepewa taarifa chini ya fungu hili na ambaye-

(a) atakosa kutayarisha kumbukumbu au kutoa habari inayota kiwa ndani ya muda au kwa namna iliyoelezwa katika taarifa hiyo; au

(b) atakayetarisha kumbukumbu au atakayetoa habari ya uwongo au ya kupotosha katika jambo lolote la maana,

atakuwa ametenda kosa na iwapo ataonekana ana hatia itabidi atozwe faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au kupewa adhabu zote mbili, faini hiyo na kifungo hicho.

SEHEMU YA TANO

MASHARTI YA FEDHA NA YA UONGOZI

18.-(1). Rais atamteua Meneja Mkuu wa Mamlaka ambaye ndiye atakayekuwa mtendaii mkuu wa Mamlaka.

Kuajiri wafa-
nyakazi

(2) Baraza, laweza mara kwa mara kuajiri watumishi wengine wa Mamlaka na kuwawekea masharti ya kazi ambayo Baraza litaona yanafaa na ambao idadi yao itaamuliwa na Baraza kutegemea mahitaji na haja ya kuhakikisha utekelezai bora wa kazi na shughuli za Mamlaka.

19.-(1) Baraza laweza kumhamisha mfanyakazi yeyote wa Mamlaka akafanye kazi katika kampuni ndogo ya Mamlaka, au kumhamisha mfanyakazi, yeyote wa kampuni, ndogo ya Mamlaka akafanye kazi katika Mamlaka au katika kampuni ndogo nyingine ya Mamlaka.

Uhamisho
wa wafanya-
kazi wa
Mamlaka

(2) Iwapo mfanyakazi anahamishwa kwa mujibu wa fungu hili, basi-

- (a) tokea tarehe ya uhamisho wake, atafahamika kama ni mfanyakazi wa kampuni ndogo au wa Mamlaka au, kadri itakavyo kuwa. mfanyakazi wa hiyo kampuni ndogo nyingine alikoha mishiwa;
- (b) masharti yake ya kazi baada ya uhamisho wake hayatakuwa magumu kuliko aliyokuwa nayo kabla ya uhamisho huo, na katika kufikiria malipo ya kiinua mgongo au faida nyingineyo yoyote ya uzeeni, utumishi wake katika Mamlaka au kadri itakavyokuwa, katika kampuni ndogo aliyohamishiwa, utafahamika kama unaendelea pamoja na utumishi wake kabla ya kupata uhamisho; na
- (C) kuajiriwa kwake kabla ya uhamisho na kuajiriwa kwake baada ya uhamisho kutafahamika kama kuajiriwa na muajiri mmoja kwa tafsiri ya fungu la 8A la Sheria ya Kiinua Mgongo, ya 1962. na Sheria hiyo itatumika kwa muajiri na muajiriwa kwa kufuata hali zilizoelezwa kwenye kifungu cha (1) cha fungu hilo.
- Sura ya 487
- Ujira wa wajumbe wa Baraza
- 20.(I) Bila kuathiri kifungu cha (2), wajumbe wa Baraza watakuwa na haki ya kulipwa ujira, posho au marupurupu kwa ajili ya gharama za matumizi ambazo Waziri ataziweka mara kwa mara kwa mapendekezo ya Baraza.
- (2) Hakuna ujira wowote, posho au marupurupu atakayolipwa mjumbe yeyote wa Baraza ambaye ni mtumishi wa Serikali isipokuwa tu yale marupurupu kwa gharama za matumizi yaliyoidhinishwa mahsusi na Waziri.
- Masilahi ya tizeeni
21. Baraza la Wakurugenzi laweza
- (a) kutoa bahashishi au masilahi mengineyo ya uzeeni kwa wafanyakazi wa Mamlaka;
- (b) kuanzisha na kuchangia kwenye mfuko wa malipo ya uzeeni au mfuko wa masilahi ya matibabu kwa ajili ya wafanyakazi wa Mamlaka;
- (c) kumtaka mfanyakazi yeyote wa Mamlaka achangie kwenye mfuko wa malipo ya uzeeni au mfuko wa masilahi ya matibabu na kuweka kima cha mchango na jinsi ya kulipa kwake.
- Uwezo wa Baraza wa kuwakilisha madaraka yake
- 22.-(1) Bila kuathiri kifungu cha (4), Baraza, mara kwa mara. na kwa hati ya maandishi yenye muhuri wa Mamlaka, laweza kuwakilisha kazi zake au uwezo wake chini ya Sheria hii kwa. Kamati yoyote ya Baraza au kwa. mfanyakazi yeyote wa. Mamlaka ili kazi na uwezo uliowakilishwa utekelezwe kwa mujibu wa. masharti ya hati hiyo.
- (2) Uwakilishaji chini ya fungu hili waweza kupewa ofisa mwenye cheo chini ya Mamlaka kwa. kutaja cheo chake bila ya kumtaja jina. lake, na kwa. hali hiyo kila. mwenye kushika. cheo hicho na. kila. mtu anayeshika au anayetenda kazi za cheo hicho, bila. ya kuhitajia ruhusa nyingine, ataweza kutekeleza kazi au uwezo uliowakilishwa kwako kwa. mujibu wa uwakilishi aliopewa.

(3) Baraza laweza, wakati wowote, kubatilisha uwakilishi uliotolewa chini ya fungu hili na hakuna chochote kitakacholizuwia kutekeleza kazi zake au uwezo wake ambao liliuwakilisha.

(4) Baraza, kamwe halitaweza kuwakilisha

(a) uwezo wake wa kuwakilisha; au

(b) uwezo wake wa kuthibitisha makadirio ya mwaka au makadirio yoyote ya ziada, mizania ya mwaka au maelezo yoyote ya hesabu.

23. Mapato ya Mamlaka yatakuwa hivi-

(a) kiasi cha fedha kitakachotolewa na Bunge kwa ajili ya Mamlaka;

(b) kiasi cha fedha ambacho Mamlaka yaweza kukopa mara kwa mara kwa mujibu wa Sheria hii;

(c) kiasi chochote cha fedha kitakachoweza kulipwa Mamlaka chini ya Sheria hii au chini ya Sheria yoyote nyingineyo ya maandishi au kitakachoingia kwenye Mamlaka kwa jinsi yoyote katika utekelezaji wa kazi zake.

Mapato ya
Mamlaka

24.-(1) Baraza laweza baada ya kupata kibali cha Waziri, na kwa idhini ya Waziri wa Fedha, mara kwa mara kukopa fedha na mikopo mingineyo kutoka kwa mtu yeyote kwa ajili ya shughuli za Mamlaka, na Baraza litakuwa na uwezo, kwa kuzingatia maagizo yoyote yatakayotolewa na Waziri kwa minajili hiyo, wa kuamua juu ya masharti yanayofaa kwa mikopo kuhusu malipo ya deni lenyewe na malipo ya riba.

Uwezo wa
kukopa na
kudhamini
mikopo

(2) Baraza laweza, iwapo linaona masilahi ya umma yahitajia hivyo, na baada ya kupata kibali cha Waziri, kudhamini malipo ya mkopo na pia malipo ya riba kwa mkopo aliopeva mtu yeyote anayejishughulisha na kilimo au uzalishaji wa kahawa au anayejishughulisha na utengenezaji au uuzaji wa kahawa au mazao yatokanayo na kahawa.

(3) Mtu anayetoa mkopo au fedha nyinginezo kwa Mamlaka, au anayetoa mkopo kwa mtu yeyote ambao malipo, yake yamedhamiiniwa na Mamlaka hatalazimika kuuliza kama Baraza limepata kibali cha Waziri kuchukua mkopo huo au fedha nyinginezo au dhamana hiyo.

25. Baraza laweza, baada ya kupata kibali cha Waziri, mara kwa mara, kutumia kiasi cha akiba ya fedha za Mamlaka, ambazo hazihitajiwi kwa wakati huo kwa shughuli za Mamlaka, kutegea uchumi kwa njia ambazo zimeruhusiwa kwa mujibu wa Sheria ya hifadhi ya Mapato ya Wadhamini ya mwaka 1967.

Kutegea
uchumi

Sheria za
1967, Na 33

26.-(1) Bila kuathiri kifungu cha (2), "mwaka" katika Sheria hii maana yake ni kipindi cha muda usiozidi miezi kumi na mbili mfululizo kitakachoteuliwa na Baraza kuwa ndicho kipindi cha mahesabu cha Mamlaka.

Makadirio
ya mapayo
na
matumizi

(2) Mwaka wa kwanza wa Mamlaka utanza mnamo tarehe ya kuanza, na waweza kuwa mwaka wa kipindi cha muda unaozidi au kupungua miezi kumi na mbili

(3) Ndani ya miezi miwili kabla ya mwaka wowote mpya kuanza (isipokuwa mwaka wa kwanza) Baraza litajadili, katika mkutano. na, kupitisha makadirio ya mapato na matumizi (makadirio ambayo kwa kifupi yataitwa "makadirio ya mwaka") ambayo yataeleza kinaganaga Mamlaka yatazamia katika mwaka huo-

- (a) kupata kiasi gani cha fedha; na
- (b) kutumia kiasi gani cha fedha,

na iwapo hali ya mambo italizimu hivyo, basi Baraza litapitisha makadirio ya nyongeza katika mwaka, wowote.

(4) Makadirio ya mwaka yote na makadirio ya nyongeza yote yatatakiwa kuwa. na maelezo kamili kadri Waziri atakavyoidhinisha.

(5) Mara tu baada ya kupitisha makadirio ya mwaka yoyote au makadirio ya nyongeza yoyote. Baraza litawasilisha, kwa, Waziri makadirio ya mwaka hayo au, kadri itakavyokuwa, makadirio ya nyongeza hayo ili atoe kibali chake.

(6) Baada ya kupokea makadirio ya mwaka au makadirio ya nyongeza Waziri aweza kuyakubali au kuyakataa au aweza kuyarekebisha kwa namna yoyote atakayoona inafaa.

(7) Baada ya Waziri kuyakubali makadirio ya mwaka yoyote au makadirio ya nyongeza yoyote ama bila mabadiliko ama baada ya kuyarekebisha, basi, bila kuathiri kifungu cha (8), Baraza litatakiwa kufuata makadirio hayo na itakuwa marufuku kutumia kiasi chochote cha fedha kwa shughuli za Mamlaka kinachozidi makadirio yaliyopangwa na kukubaliwa na Waziri.

(8) Baraza laweza

- (a) kwa kibali maalum kilichotolewa kwa maandishi na Waziri, kutumia kiasi chochote cha fedha hata kama, kiasi hicho hakikupangwa katika makadirio ya matumizi;
- (b) kurekebisha matumizi kwa ajili ya kukabili matatizo ambayo haikuwezekana kuyafikiria wakati wa kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi, ila kwa sharti kwamba, Baraza litawasilisha kwa Waziri makadirio ya nyongeza ndani ya, miezi miwili tangu yaliporekebishwa matumizi hayo.

Hesabu na ukaguziwa hesabu

27.-(1) Baraza litaangalia kuwa hesabu kamili na sahihi zinatengenezwa na. kuwekwa kuhusu-

(a) mapato na matumizi ya Mamlaka, pamoja na mambo mengine yote yanayohusika na fedha au mali za. Mamlaka;

(b) rasilimali na madeni ya Mamlaka, na. litahakikisha kuwa kunatengenezwa kila mwaka mizania itakayoonyesha mapato na matumizi ya Mamlaka. pamoja na maelezo ya rasilimali yake na. madeni yake.

(2) Baada ya mwisho wa. kila mwaka na ndani ya, miezi sita tangu mwisho wa mwaka vitabu vya hesabu vya Mamlaka pamoja na mizania ya mwaka huo vitatakiwa vikaguliwe na Shirika la Tanzania la Ukaguzi wa Hesabu lililoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Shirika. la Tanzania la Ukaguzi wa Hesabu, ya mwaka 1968.

Sheria za 1968, Na. I

(3) Kila mizania iliyokaguliwa itawasilishwa mbele ya mkutano wa Baraza na ikiwa Baraza litaikubali mizania hiyo basi Baraza lita-thibitisha kwa maandishi kwamba taarifa hiyo imekubaliwa na Baraza.

(4) Mara tu baada ya vitabu vya hesabu vya Mamlaka vikisha-kaguliwa, na kwa hali yoyote ndani ya miezi sita. tangu mwisho wa mwaka. Baraza litapeleka kwa, Waziri nakala moja ya taarifa ya Ukaguzi wa vitabu hivyo vya hesabu pamoja na nakala moja ya taarifa ya wakaguzi wa hesabu. kama ipo, kuhusu ukaguzi waliofanya na matokeo yake.

28.-(1) Kila baada ya mwisho wa mwaka na ndani ya miezi sita tangu mwisho wa mwaka Mamlaka itaangalia kuwa taarifa ya mwaka ambayo itaeleza kwa, jumla kuhusu kazi na shughuli za Mamlaka, katika mwaka huo itatengenezwa na kupelekwa kwa Waziri. Kutaa-mbatishwa kwenye taarifa hiyo-

Taarifa ya
mwaka

- (a) nakala moja ya hesabu za Mamlaka zilizokaguliwa, pamoja na taarifa ya wakaguzi wa hesabu kama ipo, kuhusu hesabu hizo;
- (b) orodha ya maagizo yote ambayo Waziri aliyatoa kwa Mamlaka katika mwaka huo kwa mujibu wa Sheria hii;
- (c) habari yoyote nyingine kadri Waziri atakavyoagiza.

(2) Mamlaka pia yatampelekea Waziri taarifa nyinginezo kuhusu mambo yake ya fedha kadri atakavyoagiza mara kwa mara kwa maandishi.

(3) Mapema iwezekanavyo baada ya kuzipokwa, Waziri atawasilisha mbele ya Bunge hesabu za Mamlaka zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya wakaguzi wa hesabu, kama, ipo, kuhusu hesabu hizo na taarifa ya mwaka ya Mamlaka.

29.-(1) Waziri aweza, baada ya kushauriana na Waziri wa Fedha pamoja na Baraza, kwa kutangaza amri katika *Gazeti la Serikali*, kuamuru kuwa ushuru utozwe kwa kahawa au kwa aina yoyote ya kahawa inayolimwa au inayotengenezwa katika Jamhuri ya Muungano.

Uwezo wa
kutoza
ushuru

(2) Kiasi cha ushuru utakaotuzwa kwa mujibu wa fungu hili kita-kadiriwa na kukusanywa kama itakavyoagizwa kwenye kanuni zita-kazotungwa kwa mujibu wa Sheria, hii na. ushuru huo utakuwa ni moiawapo ya njia za Mamlaka kupatia mali.

SEHEMU YA SITA

MASHARTI YA KAWAIDA

30. Bila kuathiri masharti ya fungu la 284A la Sheria ya Kanu, ni za jinai au masharti ya Sheria, ya Madeni ya Watumishi wa Serikali, ya mwaka 1970 au masharti ya Sheria ya Madeni ya Watumishi wa Mashirika ya Umma, ya 1974, mjumbe yeyote wa Baraza au mtumishi yeyote wa. Mamlaka. atakayetenda jambo lolote au atakayekosa kutenda jambo lolote linalohusika na madaraka yake kama mjumbe wa Baraza au mtumishi wa Mamlaka, akitenda au akikosa kutenda jambo hilo kwa nia njema, na kwa mujibu wa. Sheria, hatakuwa. na lawama yoyote ya kustahili kuchukuliwa, hatua. za kisheria kutokana na jambo hilo.

Dhamana ya
wajumbe wa
Sura ya 16
Sheria za
1970 Na .7
Sheria za
1974, na 37

Uwezo wa kupekua

31.-(1) Iwapo Polisi yeyote mwenye cheo cha, Mkaguzi Msaidizi au cheo cha juu zaidi ya hicho, au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na Mamlaka kwa maandishi kwa ajili hiyo, atatuhumu kwamba kahawa yoyote inashughulikiwa au irreshughulikiwa kinyume cha kanuni zozote, amri, maagizo au matakwa yoyote yaliyotungwa, au yaliyotolewa au kuwekwa kwa mujibu wa Sheria hii. aweza, bila kuathiri kanuni zozote zilizowekwa kwa minajili hiyo-

- (a) kusimamisha au kuingia na kupekua gari au chombo chochote kinachotumiwa kusafirisha kahawa; au
- (b) kuingia na kupekua mahali popote panapotumiwa kwa ukulima, utoaji, ufanyaji, uwekaji au utengenezaji wa kahawa; au
- (c) kuingia na kupekua mahali popote ambapo panawekwa vitabu vyovyote au hati zozote zinazohusikana na shughuh za kahawa.

kwa madhumuni ya kufanya upelelezi kuhusu kosa lolote dhidi ya Sheria hii na anaweza kuikagua, kuipima kwa mizani au kuikadiri kahawa yoyote itakayopatikana na pia kuchukua nakala za vitabu vyovyote au hati zozote au kuchomoa na kuchukua kurasa za vitabu hivyo au sehemu za hati hizo.

(2) Mtu yeyote atakayenikaidi au kumzuia ofisa yeyote wa polisi au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa fungu hili atakuwa ainetenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu mbili au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi sita au kupewa adhabu zote mbili, faini hiyo na kifungo hicho.

Adhabu ya jumla

32. Iwapo mtu yeyote atatenda kosa lolote dhidi ya Sheria hii au dhidi ya sheria ndogo zozote zilizotungwa kwa mujibu wa Sheria hii, ambalo halikuwekwa adhabu maalum, akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au kupewa adhabu zote mbili, faini hiyo na kifungo hicho.

Kuhozi

33.-(1) Iwapo mtu yeyote atapatikana na hatia kwa kosa lolote dhidi ya Sheria hii au dhidi ya sheria ndogo zozote zilizotungwa kwa mujibu wa Sheria hii, pamoja na adhabu yoyote atakayopewa mtu huyo, mahakama yaweza kuamuru kuwa ile kahawa inayohusika katika kosa hilo ichukuliwe na Mamlaka.

(2) Kahawa yoyote itakayochukuliwa kwa mujibu wa fungu hili itakabidhiwa Mamlaka na itakuwa mali ya Mamlaka bila gharama zozote na Mamlaka hayatahusishwa na rehani, madeni au viziwi vingine vyovyote, ilivyowahi kuwekwa kahawa hiyo.

Kosa kutendwa na shirika

34. Iwapo kosa lolote dhidi ya Sheria hii au dhidi ya sheria ndogo zozote zilizotungwa kwa mujibu wa Sheria hii litatendwa na shirika, basi pamoja na shirika hilo mtu yeyote ambaye, wakati lilipotendeka kosa, alikuwa ndiye mkurugenzi au ofisa aliyesimamia mambo ya shirika hilo naye pia atakuwa ametenda kosa hilo na atastahili kushtakiwa na kuadhibiwa ipasavyo, isipokuwa tu kama atathibitisha na kuitosheleza mahakama kwamba yeye hakujua, na hata kama angejitahidi vyovyote vile kutaka kujua asingewciza kujua kuwa kosa linaendeka.

- 35.** Iwapo mtu yeyote ambaye ni muwakilishi au ni mtumishi wa mtu mwingine atatenda. kosa, dhidi ya, Sheria hii au dhidi ya sheria ndogo zozote zilizotungwa. kwa mujibu wa, Sheria.hii, basi pamoja na muwakilishi au mtumishi huyo, msimamizi au muajiri naye pia. atakuwa ametenda, kosa. hilo na. atastahili kushtakiwa, na. kuadhibiwa, ipasavyo, isipoku wa tu kama atathibitisha na kuitosheleza mahakama kwamba, yeye hakujua, na hata kama. angejitahidi vyovyote vile kutaka kujua. asingeweza, kujua, kuwa. kosa. linatendeka.
- Muajiri au msimamizi kuhusika na kosa
- 36.** Iwapo amri yoyote au agizo lolote lililotolewa na. Waziri, Mkurugenzi au Mamlaka, chini ya. Sheria. hii halihitaii kutanpza katika Gazeti la Serikali, basi amri hiyo au agizo, hili litafikishwa kwa watu wanaohusika au wanaoelekea kuhusika na, kanuni au agizo hilo kwa njia yoyote itakayoteuliwa na Waziri, Mkurugenzi au, kadri itakavyokuwa, na Baraza:
- Utangazaji wa kanuni au maagizo
- Isipokuwa. kwamba, iwapo, amri hiyo au agizo hilo litatangazwa katika *Gazeti la Serikali*, itafahamika kuwa watu wote wana. taarifa. kuhusu amri hiyo au agizo hilo.
- 37.** Katika mashauri yoyote yanayohusu kosa dhidi ya Sheria, hii jukumu la kuthibitisha kuwa mshtakiwa hahusiki na amri, agizo au sharti ambalo kwalo kosa. analoshtakiwa, kuwa. amelitenda, limetendeka au, iwapo amri, agizo au sharti hilo, halikutangazwa katika *Gazeti la Serikali* jukumu la kutibitisha kuwa hakuwa na, taarifa ya mambo yaliyokuwamo, katika. amri, agizo au, kadri itakavyokuwa, sharti hilo litakuwa ni jukumu la mshtakiwa.
- Jukumu la kuathitisha
- 38.** Waziri, au kwa, kibali cha Waziri, Mamlaka, yaweza kumsamehe mtu yeyote au aina yoyote ya watu, au kuisamehe kahawa au aina. yoyote ya kahawa. kuhusikana na. masharti yote au masharti fulani ya. kanuni yoyote, amri, agizo au sharti lolote lililotungwa, au lililo,wekwa. au kutolewa, kwa, mujibu wa Sheria, hii.
- Msamaha
- 39.**-(1) Waziri aweza kuweka kanuni kwa, ajifi ya. utekelezaji bora wa madhumuni na masharti ya. Sheria hii.
- Waziri kuweka kanuni
- (2) Bila ya kuathiri uwezo huo wa jumla uliotolewa na kifungu cha (1), Waziri aweza kuweka kanuni zinazohusu-
- uendeshaji wa kazi za Mamlaka na za Baraza;
 - Baraza kuteua kamati za Baraza ambazo mikutano yake, inaweza kuhudhuriwa na watu wasiokuwa wajumbe wa Baraza kwa kuaribishwa;
 - kazi za Meneja Mkuu;
 - masharti yatakayotumika katika kuwapatia wakulima, watengenezaji wa kahawa na watu wengine misaada au huduma zozote zilizotajwa ambazo zinahusiana na kazi za Mamlaka;
 - kupiga marufuku au kudhibiti uingizaji wa kahawa nchini au upelekaji nje wa kahawa;
 - udhibiti na urekebishaji wa ununuzi, uuzaji na utengenezaji wa kahawa;

- (g) usimamlaii bora, udhibiti na uongozi bora wa Mamlaka; na kuhusu masharti na kurekebisha nidhamu ya watumishi wa Mamlaka;
- (h) kitu chochote ambacho kwa mujibu wa Sheria hii inabidi au inaruhusiwa kuwekewa kanuni, na zinazohusu jambo jingine lolote ambalo kwa maoni ya Waziri ni lazimia litajwe katika kanuni ili kuleta ufanisi katika shughuli za Mamlaka.
- (3) Kanuni zitakazotungwa kwa mujibu wa fungu hili itabidi zitangazwe katika *Gazeti ita Serikali*.

SEHEMU YA SABA

KUVUNJWA Kwa BARAZA LA KAHAWA NA MATOKEO YAKE

Ufafanuzi

40. Katika sehemu hii na katika Sehemu ya VIII ila iwapo maelezo yatahitajia vinginevyo, "Baraza la Kahawa" maana yake ni Baraza la Kahawa la Tanganyika lililoanzishwa na Sheria ile ya zamani ya Uchumi wa Kahawa.

Kuhaw,lisha rasilimali na dhima za Baraza la Kahawa

41. Kuanzia tarehe ya kuanza, msilimali yote na dhima zote za Baraza la Kahawa, kwa mujibu wa fungu hili na bila ya uhakikisho zaidi, zitakuwa ni za Mamlaka, na Baraza la Kahawa litakuwa limevunjwa.

Matokeo ya kuvunjwa kwa Baraza la Kahawa

42.-(1) Kila mtu ambaye mam tu kabla ya tarehe ya kuanza aliajiriwa na Baraza la Kahawa ataajiriwa na. tangu tarehe hiyo Mtu huyo atafahamika kama anaajiriwa na Mamlaka.

(2) Mtu akishakuwa mtumishi wa Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha (1), masharti yake ya kazi akiwa mtumishi wa Mamlaka hayatakuwa magumu zaidi, ila tu iwapo Rais ataagiza vinginevyo, kuliko yale aliyopasika nayo mam tu kabla ya kuhamishiwa kwenye utumishi wa Mamlaka na itafahamika kwamba mtu huyo ameteuliwa kuwa mtumishi wa Mamlaka katika nafasi ambayo Baraza litaamua, na kwa madhumuni ya kukadiria haki yake yoyote ya kiinua mgongo au masilahi mongineyo ya uzeeni, utumishi wake katika Mamlaka utahesabiwa kama unacadelea pamoja na utumishi wake kabla ya tarehe ya kuanza.

(3) Mtu akishakuwa mtumishi wa Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha (1), utumishi wake mara kabla ya tarehe ya kuanza na utumishi wake katika Mamlaka utafahamika kama ni utumishi unaoendelea chini ya muajiri mmoja kwa mujibu wa fungu la 8A la Sheria ya Kiinua Mgongo, ya mwaka 1962, na pia Sheria hiyo itatumika kwa wote wanaohusika kwa namna ile ile kama inavyotumika kwenye, hali zilizoelzwa katika kifungu cha (1) cha fungu hilo.

(4) Kila hati iliyotaiwa chini ya kifungu cha (5) na ambayo inahusika kwenye kifungu hicho, basi kwa mujibu wa kifungu hiki itaendelea kuwa na nguvu kamili na maana, na mamlaka-

- (a) yatasimama badala ya Baraza la Kahawa kuwa ni yenyo kuhusika kwenye hati hiyo-,

- (b) yatakuwa na haki ya kupokea fedha yoyote na kulazimisha malipo ya fedha yoyote inayopasa kulipwa kwa mujibu wa hati hiyo;
- (c) yatakuwa na haki ya kupata na kulazimisha ipatikane mali yoyote inayohawilishiwa, inayoletwa au inayotolewa au ambayo inapasa kuhawilishiwa, kuletwa na kutolewa kwa mujibu wa hati hiyo;
- (d) yatapaswa kulipa fedha yoyote inayopasa kulipwa kwa mujibu wa hati hiyo.
- (e) yatapaswa kuhawilisha, kupeleka au kutoa mali yoyote inayopasa kuhawilishwa, kupelekwa au kutolewa kwa mujibu wa hati hiyo.
- (5) Kifungu hild kinahusika na hati (pamoja na hati za mikataba, dhamana, mapatano, idhini, rehani, matozo, hawala, drafu za benki cheki, hati za fedha na za amana-
- (a) ambazo Baraza la Kahawa linahusika nazo;
- (b) ambazo kwazo fedha yoyote italipwa au itabidi ilipwe au mali nyingine yoyote itahawilishwa, itatolewa au kugawanywa au itabidi ihawilishwe, itolewe au igawanywe na Baraza la Kahawa, ambazo zilikuwapo mnamo tarehe ya kuanza au ambazo zitaanza kuwa na nguvu baada ya tarehe hiyo.
- (6) Kila mahali katika Sheria yoyote panapotajwa Baraza la Kahawa ifahamike kuwa Mamlaka ndiyo inatajwa.

SEHEMU YA NNE

KUFUTWA KWA SHERIA YA KAHAWA YA ZAMANI NA MATOKFO YAKE

- 43.**-(1) Sheria ya Kahawa ya zamani sasa imefutwa.
- (2) Kila leseni aliyopewa mtu yeyote chini ya Sheria ya Kahawa ya zamani ili imruhusu kujishughulisha na kahawa kwa namna yoyote ile, tangu tarehe ya kuanza, itafahamika kuwa leseni hiyo imefutwa.438
- 44.** Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria ya Kahawa ya zamani-
- (a) maagizo yote yaliyotolewa mtu yeyote chini ya sheria ya kahawa zilizotungwa na Waziri kwa mujibu wa Sheria ya Kahawa ya zamani, ambazo zitakuwa bado zinatumika mnamo tarehe kuanza zitafahamika kuwa ni maagizo yaliyotolewa na Mamlaka au kadri itakavyokuwa, kuwa ni kanuni zilizotungwa na Waziri kvVi mujibu wa Sherla hii, na zitaendelea ku-tumika mpaka zitakapofutwa kwa maagizo au kanuni zitakazotungwa kwa mujibu wa Sheria hii:

Kufutwa kwa sheria ya kahawa ya zamani, sura 438

Masharti ya sheria ya kahawa ya zamani yatakayo endelea kutumika

Isipokuwa kwamba fasili hii haitayahusu maagizo yoyote au kanuni zozote zinazohusika na leseni kwa ajili ya kushughulika na kahawa au kuhusu utozaji na ukusanyaji wa ushuru,;

- (b) kila amri ya kulazimisha kuuza kahawa iliyotolewa na Baraza la Kahawa kwa mujibu wa Sheria ya Kahawa ya zamani ambayo itakuwa bado Inatumika mnamo tarehe ya kuanza itafahamika kuwa ni amri iliyotolewa na Namlaka kwa mujibu wa Sheria hii hadi hapo itakapofutwa au kubadilishwa kwa,amri, itakayotolewa kwa mujibu wa Sheria hii.

Masharti
ya muda

45.-(1) Bila ya kujali sharti lolote la kinyume katika Sheria hii, Waziri, kwa mapendekezo ya Baraza na baada ya kutosheka kuwa ziko sababu maalum ambazo kwa haki inabidi afanye hivyo, aweza kumruhusu mtu yeyote aliyepewa leseni kwa Mujibu wa Sheria ya Kahawa ya zamani ashughulike na kahawa, aendeele na shughuli zake baada ya tarehe ya kuanza. kwa masharti atakayoyaweka Wazin:

Isipokuwa kwamba uwezo aliopewa Waziri na fungu hili hautatumika baada ya kupita muda wa miezi sita tangu tarehe ya kuanza.

(2) Wakati wowote kabla ya miezi kumi na mbili kupita tangu tarehe ya kuanza, Waziri aweza, kwa kutangaza amri katika *Gazeti la Serikali*, kuweka masharti yoyote ya muda, au ya nyongeza atakayo-yaona ni ya lazima yafuatie kufutwa kwa Sheria ya Uchumi wa Kahawa ya zamani au kwa kuyawezesha Mamlaka kuchuku. a msilmali na dhima za Baraza la Kahawa kwa urahisi zaidi.

NYONGEZA

(Fungu la 5 (2))

Muundo wa
Baraza

1.-(I) Baraza litakuwa na wajumbe wafuatao-
(a) Mwenyekiti, ambaye atateuliwa na Rais;
(b) Meneja Mkuu;
(c) waiumbe wengineo wasiopungua kumi na wasiozidi kumi na mbili watakaoteuliwa na Waziri.
(2) Wajumbe watakaoteuliwa kwa mujibu wa fasili ya (c) watakuwa ni watu ambao Waziri anawaona kuwa wanao ujuzi katika uzalishaji na uuzaji wa kahawa au mazao yatokanayo na kahawa, wenye ujuzi katika mambo ya fedha, uongozi au katika mambo yanayohusu mipango ya uchumi au maendeleo.
(3) Baraza laweza kumchagua mjumbe yeyote wa Baraza au mtumishi yeyote wa Mamlaka kuwa Katibu wa Baraza.

Makamu
wa
Mwenyekiti

2. Wajumbe wa Baraza watamchagua mmoja wao awe Makamu wa Mwenyekiti wa Baraza, na miumbe yeyote atakayechaguliwa kuwa Makamu wa Mwenyekiti, iwapo ataendelea kuwa miumbe, atashika cheo, hicho kwa muda wa mwaka mmoja tokea tarehe ya kuchaguliwa kwake, na atakuwa na haki ya kuchaguliwa tena.

Muda wa
kuwa
mjumbe

3.-(1) Mjumbe wa Baraza, isipokuwa Meneja Mkuu, kama hataondolewa mapema na yule mwenye madaraka ya kuteua, au kama hataacha kuwa mjumbe kwa njia nyingine yoyote ile, atakuwa miumbe kwa muda uliotaiwa na mwenye madaraka ya kuteua katika hati ya uteuzi wake na, kama hakuna muda uliotajwa, basi atakuwa mjumbe kwa muda wa miaka mitatu tangu tarehe ya kuteuliwa kwake, na atakuwa na haki ya kuteuliwa tena.

(2) Mjumbe yeyote wa Baraza, isipokuwa Meneja Mkuu, aweza kujiuzulu wakati wowote kwa kumpelekea taarifa ya maandishi mwenye madaraka ya kuteua, na tokea tarehe iliyotajwa katika taarifa hiyo au, kama haikutajwa, tokea tarehe ya kupokelewa taarifa hiyo na mwenye madaraka ya kuteua, ataacha kuwa miumbe.

Uteuzi wa
mjumbe
wa muda

4. Iwapo mjumbe yeyote wa Baraza, isipokuwa Meneja Mkuu, kwa sababu ya kutokuwapo katika Jamhuri ya Muungano au kwa sababu ya ugonjwa au kwa sababu nyingine yeyote yenye maana hataweza kufanya kazi zake za ujumbe wa Baraza, -basi mwenye madaraka ya kuteua aweza kumteua mjumbe wa muda ashike mahali pake. na mjumbe huyo wa muda atakuwa mjumbe mpaka yule mjumbe wa kudumu atakapo reja kazini au mpaka muda wa mjumbe wa kudumu utakapomalizika.

5.-(1) Baraza, kwa kawaida, litakutana mnamo saa na mahali patakapochaguliwa na Baraza kwa ajili ya kujadili shughuli zao na, lakini kwa yeyote vile, litakutana ya walau mara moja kwa kila miezi mitatu.

Mikutano
ya Baraza

(2) Mwenyekiti, au akiwa hayupo Makamu wa Mwenyekiti, aweza kuitisha mkutano maalum wa Baraza wakati wowote, na ataweza kuitisha mkutano maalum kwa ombi la maandishi kutoka kwa wajumbe walio wengi wa Baraza.

(3) Mwenyekiti, au akiwa hayupo Makamu wa Mwenyekiti, ataongoza kila mkutano wa Baraza. Iwapo Mwenyekiti na Makamu wa Mwenyekiti wote wawili hawapo, basi wajumbe waliohudhuria watamchagua mmoja wao aongoze mkutano huo.

6. Kiwango cha mkutano wa Baraza kitakuwa watu saba.

Kiwangi
cha
Mkutano

7.-(1) Mambo yanayojadiliwa kwenye mkutano wa Baraza yataamuliwa kwa kura zilizo nyingi za wajumbe waliohudhuria na wanaopiga kura, na itokeapo usawa wa kura, basi mtu anaongoza mkutano huo atapiga kura ya pili au ya uamuzi.

Uamuzi wa
Baraza

(2) Bila ya kujali kifasili cha (1), Baraza laweza kutoa uamuzi bila ya kuitisha mkutano kwa kuwapelekea wajumbe wa Baraza karatasi zinazohusika na kupata maoni ya walio wengi kwa maandishi, lakini mjumbe yeyote aweza kutaka uamuzi uahirishwe najambo bilo lifikiwiwe kwenye mkutano wa Baraza.

8. Baraza litaangalia kuwa kumbukumbu za mikutano yake yote zinaandikwa au kuwekwa, na kumbukumbu ya kila mkutano wa Baraza zitathibitishwa na Baraza kwenye mkutano utakaofuata na kutiwa sahihi na mwenyekiti wa mkutano huo.

Kumbu-
kumbu za
mikutano
nafasi wazi,
n.k hazita-
athiri
shughuli za
Baraza
Kuthibitisha
mikataba
n.k

9. Nafasi iliyoko wazi miongoni mwa nafasi za wajumbe na hata hitilafu yoyote katika uteuzi wa mjumbe yeyote kati yao haitaathiri kitendo chochote au mijadala yoyote ya Baraza.

10.-(1) Sahihi za watu wawili ndizo zitakazothibitisha muhuri rasmi wa Mamlaka, nazo ni-

(a) sahihi ya Mwenyekiti wa Baraza au ya mjumbe mwingine yeyote wa Baraza, isipokuwa Meneja Mkuu, aliyeidhinishwa na Baraza kutia sahihi; na

(b) sahihi ya Meneja Mkuu au ya mtumishi yeyote wa Mamlaka mwingine aliyeidhinishwa na Baraza kutia sahihi badala ya Meneja Mkuu.

(2) Kila hati inayotiwa sahihi na mtu binafsi au mkataba unaoingiwa na mtu binafsi ambaye si shirika la kisheria, hautahitaji kupigwa muhuri rasmi wa Mamlaka, lakini utaweza kutiwa sahihi na Meneja Mkuu au miumbe mwingine yeyote wa Baraza kwa niaba ya Mamlaka, iwapo mjumbe huyo alikwishaidhinishwa na Baraza, kwa jumla aa katika hali maalum, kuitia sahihi hati hiyo au kuingia katika mkataba huo kutokana na uamuzi wa Baraza.

(3) Kila hati inayohesabiwa kuwa ni hati iliyotiwa sahihi au iliyotolewa na Mamlaka au kwa niaba ya Mamlaka na-

(a) iliyopigwa muhuri rasmi wa Mamlaka wenye kuthibitishwa kwa jinsi iliyoelezwa kwenye kifasili cha (1); au

(b) iliyotiwa sahihi na Meneja Mkuu au mjumbe wa Baraza aliyeidhinishwa kutia sahihi kwa mujibu wa kifasili cha (2), basi hati hiyo itahesabiwa kuwa imetiwa sahihi na kutolewa karna hivyo mpaka ithibitike kinyurne cha hivyo.

11. Bila kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Nyongeza hii, Baraza linaweza kuweka na kufuata utaratibu wake wa kuendesha shughuli zake.

Uwezo wa
Bazara wa
kuendesha
shughuli
zake

Imepitishwa katika Bunge tarehe ishirini na saba prili, 1977.

Katibu wa Bunge